

## 34. Katika Tawba Ulimi Ndiyo Mfasiri Wa Moyo

Katika *TAWBA*, kama tulivyokwisha elezea hapo awali kuwa kitu cha lazima ni kusikitika na kuhuzunika kwa mtu, vile vile kujuta kwa moyo wake wote pamoja na kunuia kwake kuacha madhambi hayo na yote mengineyo. Na katika hisia hizo nzito atamke maneno mazito ya kuomba msamaha wa Allah swt na kusema: 'Astaghfirullah Rabbi wa atubu Ilayhi.'

*TAWBA* haiwezi kuwa *TAWBA* iwapo itatamkwa mdomoni tu bila ya kuwapo kwa hisia za moyoni. Hivyo inatubidi tuuelekeze ulimi wetu katika *TAWBA* baada ya kujengwa kwa hisia za moyoni kwani ulimi ndio utakao fasiri yaliyo moyoni mwetu. Ndipo hapo *TAWBA* yetu itakuwa ni sahihi.

Mfano, ninajuta na kusikitika kwa kusema matusi na maneno machafu moyoni mwangu, lakini ulimi wangu bado unaendelea na kuyasema hayo hayo. Basi katika hali kama hii, ulimi haujawa mfasiri wa moyo wangu. Utakuwa mfasiri pale utakapoacha kuyasema maneno hayo na mengineyo pia.

Hivyo tuombe Tawfiki ya kujaaliwa ulimi wetu uwe mfasiri wa moyo wetu ili kutukamilishia *TAWBA* kimoyo na kimatendo. Vile vile juhud zetu pia zinahitajika, katika kujielekeza huko.

Ipo hadithi Tukufu isemayo:

"*Adda'i bila Aamal kar-raami bila watr*" Yaani:

Mwombaji bila matendo ni sawa na upinde bila kamba yake, au mti bila matunda, au mto bila maji. Sasa tuijulize iwapo tutaomba tu bila kujitahidi wenyewe itakuwaje?

---

### Source URL:

<https://www.al-islam.org/tawba-ayatullah-sayyid-abdul-husayn-dastghaib-shirazi/34-katika-tawba-ulim-ndiyo-mfasiri-wa-moyo#comment-0>